

# Maswali Yanayoulizwa Mara Nyingi Kuhusu Chanjo ya COVID-19

**Chanjo ni mafanikio pekee ya kisayansi ambayo yamerefusha zaidi urefu wa wastani wa kuishi. Chanjo ndiyo njia pekee ya kumaliza janga hili na kurudi kwenye maisha yetu ya kawaida. Jikinge mwenyewe, wapendwa wako na jamii yako kwa kupata chanjo.**

## **Kwa nini nipate chanjo?**

Maambukizi ya COVID-19 yanaweza kusababisha kifo kwa watu wanaouguua na wenye afya nzuri wa umri wowote.

Hata ikiwa mtu hatakuwa kutokana na COVID-19, anaweza kupata matatizo ya muda mrefu ikiwa ni pamoja na kupoteza kumbukumbu, uchovu, ugumu wa kupumua usioelezeka, na uharibifu wa mapafu na moyo. Kliniki tayari zimeundwa kusaidia wagonjwa wengi wa COVID-19 ambao, ingawa hawana maambukizi tena, hawawezi kurudi kazini au kuishi maisha ya kawaida.

## **Chanjo inafanyaje kazi?**

Chanjo inafundisha kinga ya miili yetu jinsi ya kupambana na virusi na kutulinda kutokana na kuugua ikiwa tunaambukizwa COVID-19. Chanjo haiwezi kukupa COVID-19.

## **Kinga ya jamii ni nini na kwa nini ni muhimu?**

Ikiwa watu wa kutosha wana kinga, kuna uwezekano mdogo wa virusi kuenea. Tunahitaji kutoa chanjo kwa asilimia 70 hadi 80 ya watu ili kufikia kinga ya jamii na kurudi kwenye maisha yetu ya kawaida, kufungua biashara tena, kuweza kukumbatiana na kuwatembelea wapendwa tena.

## **Tayari niliambukizwa COVID-19. Je, bado ninafaa kupata chanjo?**

Hata kama ulikuwa na COVID-19 hapo awali, haijulikani kinga yako itadumu kwa muda gani. Inawezekana kupata COVID-19 tena. Bado unapaswa kupata chanjo ili ujikinge pamoja na wengine.

## **Je, bado nitalazimika kuvaa barakoa na kuweka umbali wa kimwili baada ya kupata chanjo?**

Ndiyo. Bado ni muhimu kufuata hatua za afya ya umma hadi watu wengi wapate chanjo.

## **Itachukua muda gani kupata kinga baada ya kupokea chanjo?**

Inachukua wiki mbili baada ya dozi ya pili ili mwili kujenga kinga baada ya chanjo. Mtu anaweza kuambukizwa virusi kabla tu au baada tu ya chanjo na kuugua, kwa sababu chanjo haikuwa na wakati wa kutosha kujenga kinga.

## **Mchakato wa kuunda chanjo uliharakishwa?**

Hakuna hatua zilizorukwa, na taratibu zote za usalama zilifuatwa. Chanjo zilitengenezwa kwa haraka kwa sababu ya maendeleo ya kiteknolojia na kwa sababu sehemu zisizo za kimatibabu zinazohitaji idhini (michakato ya urasimu na uidhinishaji) zilitekelezwa haraka.

## **Kuna athari mbaya?**

Kunaweza kuwa na athari kutokana na chanjo ya COVID-19, lakini huwa ni ndogo na huisha baada ya siku chache. Athari za kawaida ni maumivu kwenye misuli, maumivu ya kichwa, na homa/kuhisi baridi.

Utafuatiliwa kwa ajili ya athari yoyote ya mzio baada ya chanjo.

## **Je, chanjo ni salama?**

Chanjo ni salama. Ni salama zaidi kupata chanjo kuliko kupata ugonjwa huu na upate athari zinazoweza kutokea za muda mrefu. Mamilioni ya Wakanada tayari wamepokea chanjo na chanjo hizo zimeonyeshwa kuwa salama. Chanjo hiyo haiwezi kubadilisha DNA yako.

Ikiwa una historia ya kupata athari kali za mzio, mfumo dhaifu wa kinga, au wewe ni mjamzito, zungumza na daktari wako kabla ya kupata chanjo.



Kwa maelezo zaidi kuhusu fursa za kuisaidia 19toZero, tafadhali wasiliana na: [info@19tozero.ca](mailto:info@19tozero.ca)  
Kwa taarifa za karibuni zaidi kuhusu chanjo, tembelea: [canada.ca/covidvaccine](https://canada.ca/covidvaccine)